Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

JIJI LA DODOMA

MTIHANI WA PRE-MOCK KIDATO CHA NNE 2021

021 KISWAHILI

MUDA: SAA 3:00 MACHI, 2021

MAELEKEZO

1.Karatasi hii ina sehemu A,B,C, na D
2.Zingatia maagizo ya kila sehemu na kila swali.
3.Majibu yote yaandikwe kwa wino wa bluu au mweusi.
4. Jibu maswali yote katika sehemu A,B,C na maswali matatu sehemu D, swali la tisa ni lazima.

SEHEMU A (Alama 10)

1.Chagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele (i) hadi (x) , kisha andika herefu ya jibu hilo.

i)Ni jambo gani linalodhihirisha umbo la nje ya kazi ya fasihi?

A. Muundo
B. Jina la kitabu
C. Fani
D. Mtindo.

ii)Ni sehemu ya neno ambayo huweza kutamkwa mara moja na kwa pamoja kama fungu moja la sauti.

A. Irabu
B. Konsonati
C. Mofu
D. Silabi

iii) leta wali kuku.hii ni aina gani ya rejista?

A)rejesta ya hotolini
b)rejesta ya hospitalin
C)rejesta ya mtaani
D)rejista ya shambani

iv)Ipi maana inayoelekeana na methali hii? ‘chanda chema huvikwa pete’

a) Mwanamke mrembo
b) Mtoto wa kike mwenye tabia njema hupendwa
c) Mtoto mzuri huvaa nguo zikampendeza
d) Bibi harusi

v) .....ni hadithi zinazozungumzia matukio ya kihistoriya.

a)ngano
b)tarihi

Search ⇢ www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

c)visasili
d)soga

vi)Mara nyingi fasihi simulizi huzingatia uwepo wa ;
a)fanani na hadhira
B)mtunzi
C)fanani
d)hadhira

vii)Upi ni mzizi wa neno anakula?
A) Kul
B) La
C) L
D) Akul

viii)Ni jambo gani linalodhihirisha upekee wa kazi Fulani ya kifasihi?
a)muundo wa kazi husika
B)wahusika wa kazi husika
c)mtindo wa kazi husika
d)jina la kazi husika

ix) Neno lipi kati ya maneno haya linaweza kudokeza mtenda au mtendwa?
a)kiunganishi
b)kihisishi
C)kielezi
D)kiwakilishi

x)Ni sifa ipi haitofautishi fasihi simulizi na fasihi andishi?
a)ukubwa
B)uwasilishwaji
C)uhifadhi
d)ueneaji

SEHEMU B (Alama 5)

2 . Oanisha sentensi za kifungu A, kwa kuchagua jibu sahihi katika kifungu B, andika jibu lako kwa usahihi katika kisanduku ulichopewa hapo chini;

KIFUNGU A	**KIFUNGU B**
i) Huonesha mpangilio wa maneno kialfabeti,jinsi yanavyoandikwa kutamkwa na maana zake. ii) Mjengo au umbo la kazi ya fasihi. iii) Maneno yasiyo sanifu yanayozungumzwa na kikundi kidogo cha watu. iv) Taauluma inayoshughulikia maumbo au mjengo wa maneno katika tungo. v) Ni mtindo wa lugha inayozungumzwa kulingana na muktadha na kusudi maalum.	a) Tanzu za fasihi. b) Rejesta . c) Misimo. d) Sarufi maumbo. e) Misimu. f) Mofimu. g) Muundo. h) Nomino. i) Kamusi.

Search ⇢ www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

KIFUNGU:A	I	II	III	IV	V
KIFUNGU B					

SEHEMU C: ALAMA 40;

Jibu maswali yote katika sehemu hii

3Eleza maana ya kielezi kwa kutoa mfano wa sentensi moja.

4 Kwa kila tungo uliyopewa pigia mstari kielezi na kisha taja ni kielezi cha aina gani?

i)Darasani kuna utulivu mkubwa.

ii) Wanafunzi wanaimba kimasihara.

iii) Mwalimu amerudi tena.

iv) Nitaondoka wiki ijayo.

5. Toa maana tano(5) za neno " Kibao" kisha tunga sentensi moja kwa kila maana ulitoa.

6.Taja njia nne (4) zitumikazo kuunda misamiati na utoe mfano kwa kila njia.

7. Taja aina mbili za Mashairi na maana zake.

8 . Soma shairi lifuatalo kisha jibu sehemu hii.

Utu wa binadamu, ni kama yai na kuku,
Utu niile nidhamu,mola aliyo kukhuluku,
Ubinadamu ni damu,ya utu wa kila siku,
Utu wowote wa mtu,ni kuwajali wenzake.

Yeyote mwanadamu, ana asili ya mtu,
Yaani kwenye yake damu, hakikosi hiki kitu,
Utu sifa maalum,ya mtu kuitwa mtu,
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake.

Utu ni kiumbe hai, tunacho chaonekana,
Utu kamwe haudai, tabia ya kujivuna,
Utu ni ule uhai,ushikao uungwana.
Utu wowote wa mtu ni kuwajali wenzake

Utu unayo aibu, na tabia ya muhali,
Utu huenda na jibu,kila imani na ukweli,
Utuwe hauna tabu,tabia ya ujalili,
Utu wowote wa mtu,ni kuwajali wenzake.

MASWALI

a) Pendekeza kichwa cha shairi ulilosoma
b) Eleza maana ya maneno yaliyopigiwa mstari kama yalivyotumika katika shairi ulilosoma.
   i Kukhuluku
   ii Uungwana
   iii ujalili.

Search ⇢ www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

iv Muhali.

c) Mwandishi anasisitiza nini katika utanzu huu wa shairi
d) Onesha muundo na mtindo uliotumika katika shairi hili.
e) Umepata ujumbe gani katika shairi hili? Toa hoja mbili.

SEHEMU D(Alama 45)

Jibu maswali matatu (3) kutoka katika sehemu hii swali la 9 ni lazima

9. Ukiwa kiongozi wa michezo katika shule ya Sekondari Kizota S L P 30 Dodoma ,andika barua kwa mkuu wako wa shule kupitia kwa mwalimu wa michezo kuomba kuongezewa siku za michezo shuleni. jina lako liwe Sikunjema Afya.

10 “Msanii ni kinda la jamii husika anayoandika kuihusu jamii hiyo”. Jadili kauli hii kwa kutumia hoja tatu kutoka katika kila diwani kati ya diwani mbili zilizoorodheshwa.

11. “Wahusika katika kazi za fasihi ni mfano wa kuigwa na jamii kwa tabia na matendo yao”. Thibitisha kauli hii kwa kutumia hoja tatu kwa kila mhusika kutoka katika tamthilliya mbili zilizoorodheshwa..

12.Elimu ni ufunguo wa maisha . Fafanua kauli hii kwa kutoa hoja tatu kwa kila kitabu kati ya vitabu viwili vya riwaya vilivyoorodheshwa.

ORODHA YA VITABU

USHAIRI

Wasakatonge	M.S. Khatibu (DUP)
Malenga Wapya	TAKILUKI (DUP)
Mashairi ya Chekacheka	T.A.Mvungi (EP & D.LT.D)

RIWAYA

Takadini	Ben J. Hanson (Mbs)
Watoto Wa Mama N’tilie	E. Mbogo (H.P)
Joka La Mdimu	A.J.Safari (H.P)

TAMTILIYA

Orodha	Steve Reynolds (Ma)
Ngoswe Penzi Kitovu Cha Uzembe	E.Semzaba (Esc)
Kilio Chetu	Medical Aid Foundation(Tph)

Search ⇢ www.africona.net